Jarida la Wizara ya Afya

# Afya Habari

JARIDA LA MTANDAONI LA WIZARA YA AFYA | TOLEO, NO. 15, JANUARI 2024

TUNABORESHA AFYA
MTU NI AFYA • AFYA NI MTAJI



# TUNABORESHA AFYA

MTU NI AFYA, JALI AFYA YAKO




## BODI YA UHARIRI

**MWENYEKITI**
Dkt. John Jingu
KATIBU MKUU

**MHARIRI**
Englibert Kayombo

**MHARIRI MSAIDIZI**
Emmanuel Malegi

**WAJUMBE**
Englibert Kayombo
Emmanuel Malegi
Majid Abdulkarim
Said Nyaoza
Hassan Kimweri
Shaban Juma
Cletus Sanga
Abdulwaheed Madenge


**WASANIFU**
Englibert Kayombo
Said Nyaoza

@wizara_Afyatz
www.moh.go.tz

# YALIYOMO

Hanang chukueni tahadhari dhidi ya magonjwa ya mlipuko-dkt. Samia....UK 1





Wahudumu wa afya ngazi ya jamii ni tegemeo katika sekta ya afya .... UK 2

Wadau wa tiba asili na tiba mbadala watakiwa kusajili dawa ili zitumike katika mfumo rasmi wa hospitali .... UK 3





Majimbo 214 tanzania bara kunufaika na ugawaji wa vifaa i tiba vya shilingi bilioni 14.9.... UK 4

Waganga wafawidhi wa hospitali za rufaa za mikoa watakiwa kubainisha vipaumbele vyao kulingana na vipaumbele vya sekta 2024/25.... UK 5






Wagonjwa 6,931 kutoka nje ya nchi walitibiwa tanzania, mwaka 2023 .... UK 6

Zingatieni maadili utu na heshima katika kutoa huduma za afya..... UK 7



Serikali kuimarisha hali ya lishe kwa vijana balehe nchini .... UK 8



Kampeni ya taulo za kike milioni 5 kwa wanafunzi walipo shuleni yazinduliwa. .... UK 9

Wananchi watakiwa kuchukua tahadhari kukabiliana na ugonjwa wa kipindupindu .... UK 10



Undeni miongozo inayotekelezeka ili iwajenge uwezo watumishi na wanafunzi vyuo vya afya... UK 11

Mwaka 2023 wagonjwa 15,386 wamepata huduma mpya za ct-scan hospitali za rufaa za mikoa .... UK 12



Simamieni usafi katika maeneo yenu (kipindupindu kinaletwa na uchafu) .... UK 13

Vituo vipya 485 vya kutoa huduma za afya vimeongezeka kwa mwaka 2023.... 14



Wizara ya afya yatoa elimu kwa wanahabari juu ya ukoma .... UK 15


Wananchi chukueni tahadhari dhidi ya red eyes .... UK 16

Sekta ya afya kuendelea kuweka kipaumbele ajenda ya kupunguza vifo vya mama na mtoto .... UK 17



Rc homera aipongeza wizara ya afya kwa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.... UK 18

Zaidi ya asilimia 74 ya watanzania wanapata huduma za afya ngazi ya msingi ..... UK 19



Tanzania na wana-diaspora kuendelea kushirikiana kuboresha huduma za afya nchini .... UK 20

Msd yaanza kusambaza vifaa tiba vya huduma za afya ya uzazi katika majimbo 214 nchini..... UK 21



Wagonjwa 6,931 kutoka nje ya nchi walitibiwa tanzania, mwaka 2023.... UK 22

# Serikali imetenga bilioni 899.4 kuajiri wahudumu wa afya ngazi ya jamii 137,294

**Na. Englibert Kayombo, Dar es Salaam**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imetenga jumla ya Tsh. bilioni 899.4 kwa ajili ya kutekeleza mpango wa kuajiri na kuwajengea uwezo jumla ya Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii wapatao 137,294 katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara.

Hayo yamesemwa na Makamu wa Rais Dkt. Philip Isdori Mpango Januari 31, 2024 kwenye Uzinduzi wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii uliofanyika katika kituo cha Mkutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere Jijini Dar Es Salaam.

"Utekelezaji wa Mpango huo utafanyika katika kipindi cha Miaka Mitano kwa awamu ambapo mwaka wa kwanza 2023-2024 zaidi ya wahudumu elfu 28,000 watafikiwa na baadaye wastani wa wahudumu elfu 27,324 kila mwaka kwa kipindi cha miaka Minne mfululizo kuanzia mwaka 2024-2025 hadi 2027-2028." Amesema Makamu wa Rais Dkt. Mpango.

Aidha, Dkt. Mpango alizielekeza Wizara ya Afya, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Mamlaka nyingine zinazohusika kwa kuhakikisha kunakuwepo na usimamizi madhubuti wa Mpango Jumuishi wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii ili uweze kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Dkt. Mpango amewasihi viongozi wote wanaohusika katika ngazi zote kuhakikisha zoezi la kuwachagua wahudumu hao wa Afya ngazi ya jamii linafanyika kwa kufuata vigezo na taratibu zilizowekwa ili kupata wahudumu wenye sifa stahiki watakaotekeleza majukumu hayo na kuwataka watakaopewa jukumu la kutekeleza mpango huo, kujiepusha na vitendo vya upendeleo, rushwa au ukiukwaji wa taratibu.

"Wahudumu wa Afya mtakaopewa dhamana ya kutekeleza jukumu hili zingatieni weledi na kujituma pamoja na kutoa rai kwa jamii kuupokea mpango huo na kuthamini huduma za wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii kwa kuwapa ushirikiano wa kutosha ili kulinda na kuboresha Afya katika jamii." Amesisitiza Makamu wa Rais Dkt. Mpango.






# Wahudumu wa afya ngazi ya jamii ni tegemeo katika sekta ya afya

**Na. Hassan Kimweri,**
**Dar Es Salaam**

Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii ndio Mstari wa mbele katika Sekta ya Afya wanaoweza kuibua wagonjwa na kutoa taarifa zote kuhusu masuala ya Magonjwa ikiwemo yasiyoambukiza na yakuambukiza kama ya milipuko.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amesema hayo Januari 31, 2024 wakati wa Uzinduzi wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii iliyozinduliwa leo na Makamu wa Rais Dkt. Philip Isdori Mpango katika kituo cha Mkutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere Jijini Dar Es Salaam.

''Wahudumu wa Afya ngazi ya jamii ndio askari wa mbele katika Sekta ya Afya na ndio wanaibua wagonjwa na wanaweza wakazuia na kutoa taarifa zote kuhusu masuala ya magonjwa na ni nguzo muhimu katika kuimarisha mifumo ya Afya ngazi ya jamii ili kufikia lengo la huduma za Afya kwa wote.” Amesema Waziri Ummy

Aidha, Waziri Ummy amesema Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii wanaenda kuwapunguzia mzigo watumishi walio ngazi za Hospitali kwa kuwa kuna baadhi ya vijiji havina vituo vya Afya au vinapatikana mbali na makazi ya watu.

“Ndio maana tumeona ni muhimu sasa turasimishe mpango huu ili kutomuacha mtu yoyote, Mfano kwa upande wa ugonjwa wa Kifua Kikuu tulipoamua kutumia wahudumu wa Afya ngazi ya jamii wameibua wagonjwa wapya asilimia 50 kwa kila wagonjwa wapya 100 wanaogundulikwa na ugonjwa huo." Amesema Waziri Ummy





# Wadau wa tiba asili na tiba mbadala watakiwa kusajili dawa ili zitumike katika mfumo rasmi wa hospitali

**Na. Abdulwaheed Madenge,**
**Dodoma**

Serikali imewataka waganga na wadau wa tiba Asili nchini kusajili dawa wanazotengeneza ili ziingizwe katika mfumo wa hospitali na kuongeza masoko ya huduma jumuishi za Afya kwa kufuata mfumo rasmi wa muongozo wa dawa.

Wito huo umetolewa na Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Tiba asili Dkt. Marko Hingi wakati alipomuwakilisha Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu katika kikao cha waganga pamoja na wakuu vyama vya tiba asili na tiba mbadala Jijini Dodoma.

Katika kuendelea kuimarisha kada ya tiba asili alisema Serikali imeingiza baadhi ya dawa za tiba asili katika huduma jumuishi za Afya kwa kufuata mfumo rasmi wa muongozo wa dawa.

“Mpaka sasa Hospitali saba nchini zimeanza kutumia dawa za tiba asili na mbadala kama Huduma jumuishi za Afya kusaidia wananchi katika kupona magonjwa mbali mbali”. Amesema Dkt. Hingi.

Dkt. Hingi alisema kuwa ujenzi wa kiwanda cha NIMR Mabibo umefikia asilimia 98 na unatarajia kukamilika mapema mwaka huu.

“Kiwanda hicho kitakuwa ni jukwaa la uzalishaji wa dawa za tiba asili na mbadala hapa nchini na kusambazwa katika nchi za ukanda wa SADC“. Ameeleza.

Kwa Upande wake Mwenyekiti wa Baraza la Waganga wa Tiba Asili na Mbadala Prof. Hamisi Malebo alisema wana jukumu la kuondosha na kutibu magonjwa mbalimbali katika jamii, kuleta amani na kuisaidia Serikali kuifikia jamii.

# Majimbo 214 tanzania bara kunufaika na ugawaji wa vifaa i tiba vya shilingi bilioni 14.9




**Na Hassan Kimweri**
**Dar es Salaam**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amezindua usambazaji wa Vifaa Tiba (nje ya vilivyopangwa kununuliwa kwenye Bajeti ya 2023/24) vitakavyosambazwa katika majimbo yote 214 nchini Tanzania Bara.

Waziri Ummy Mwalimu amesema Serikali ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imetoa fedha za nyongeza Tsh. Bilioni 14.9 mwezi November 2023 na kununuliwa vifaa hivyo ili kuendelea kuboresha huduma za Afya ya uzazi, mama na mtoto.

Miongoni mwa vifaa ambavyo Waziri Ummy amepokea ni pamoja na vitanda vya wagonjwa 3,080, vitanda vya kujifungulia 1,000, magodoro 5,500, mashuka 36,808, pamoja na meza za vutanda 306.

"Tunategemea kupokea vifaa tiba vingine hivi karibuni ambavyo ni vitanda vya kujifungulia (4280), vitanda vya kufanyia uchunguzi (examination table) 4280, mkoba wa vifaa vya kujifungulia (delivery kit) 4280, kabati za vitanda (bed side lockers) 6420 na stendi ya dripu (6420)." Amesema Waziri Ummy.

Waziri Ummy amesema takwimu zinaonesha asilimia 86 ya wanawake wajawazito Tanzania wanajifungulia katika Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali za Halmashauri, vifaa hivyo vitakwenda kusaidia kuboresha huduma za Afya ya uzazi, mama na mtoto.

Amesema, katika Kila jimbo litapata Vitanda 30, Magodoro 30, Mashuka 60, Bed side locker 30, Drip Stand 30, Meza ya kulia chakula 15, Vitanda vya kujifungulia 10, Delivery set 10 pamoja na Examination bed 10.

"Waheshimiwa Wabunge watavikuta vifaa hivi kwenye vituo viwili katika kila jimbo ambapo Bohari ya Dawa (MSD) watashusha mzigo huu." Amesema Waziri Ummy

Mwisho, Waziri Ummy amemshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuiwezesha Sekta ya Afya kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuboresha huduma za afya ambapo imeweza kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

"Vifo vimepungua kutoka vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2016 hadi vifo 104 kwa vizazi hai 100,000 ikiwa lengo la Dunia ni Tanzania kupunguza vifo vya wajawazito kufikia vifo 70 kila vizazi hai 100,000 ifikapo mwaka 2030.




# Waganga wafawidhi wa Hospitali za Rufaa za mikoa watakiwa kubainisha vipaumbele vyao kulingana na vipaumbele vya sekta 2024/25

**Na Cletus Sanga,**
**Dar Es Salaam**

Waganga wafawidhi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa nchini wametakiwa kuhakikisha wanabainisha vipaumbele vya Taasisi zao kulingana na vipaumbele vya sekta ya afya kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ili kuleta ubora wa Huduma za afya nchini.

Rai hiyo imetolewa  Jijini Dodoma na Mkurugenzi wa huduma za tiba Wizara ya Afya Prof. Paschal Ruggajo katika kikao cha Waganga Wafawidhi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa kupitia Mapendekezo ya Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2024/2025.

Prof. Ruggajo amesema kuwa katika mpango wa bajeti ya mwaka 2024/25 za Hospitali zote nchini lazima ziendane na vipaumbele vya sekta ya afya ili wanachi waweze kunufaika na Huduma zinazotolewa Hospitalini.

“Lakini hakikisheni mnafanya utafiti na kutoa matokeo ya utafiti mnaofanya ili kuleta tija ya tafiti hizo kwa jamii na taifa kwa ujumla kwani tafiti pia ni sehemu ya utendaji wenu”. Amesisitiza Prof. Ruggajo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Msaidizi wa Mipango na Bajeti Wizara ya Afya Bw. Lusajo Ndagile alisema kuwa lengo la kikao hicho ni maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2024/25 pamoja na kuwajengea uwezo waganga wafawidhi hao kuandaa Mpango na Bajeti.

Pia Bw. Lusajo amesema kuwa wametumia kikao hicho kuwapitisha waganga wafawidhi hao katika mpango mkakati wa Wizara ya Afya

“Vile vile wamepata mafunzo ya muongozo juu ya Mpango na bajeti ili kuleta ufanisi wakati wa kuaanda bajeti za taasisi zao”. ameeleza Bw.Lusajo.

Aidha, Bw. Lusajo huyo amesema kikao hicho ni mwendelezo baada ya kikao cha jana kilichowakutanisha Wakurugenzi wa Fedha na Mipango kutoka Taasisi zote zilizopo chini ya Wizara ya Afya.




# Madaktari bingwa 12 wa tanzania kutoa huduma za matibabu ya magonjwa ya moyo kwa watoto nchini zambia

**Na Majid Abdulkarim,**
**Dodoma**

Serikali ya Tanzania imetuma madaktari bingwa 12 kwenda nchini Zambia kutoa huduma za kibingwa za matibabu ya moyo kwa watoto hii ikiwa ni sehemu ya kuendelea kutanua wigo wa tiba utalii na kukuza mahusiano baina ya nchi hizi mbili.

Wataalamu hao kutoka Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete(JKCI) ambao watakaa nchini humo kwa wiki mbili wanatarajiwa kutoa matibabu ya upasuaji mkubwa wa magonjwa ya moyo hususani kwa watoto chini ya miaka 15 na kuisaidia nchi ya Zambia kuanzisha huduma ya matibabu ya moyo nchini humo.

Hayo yamebainishwa na Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Mollel wakati akizungumza na vyombo vya habari juu ya huduma za mkoba (outreach services) za matibabu ya kibingwa nje ya Tanzania kutoka JKCI.

Dkt. Mollel alisema kuwa katika uwekezaji mkubwa aliofanyika katika sekta ya afya na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika teknolojia, kusomesha wataalamu, miundombinu ya hospitali imeleta mapinduzi makubwa mpaka Tanzania kuwa kitovu cha tiba utalii Afrika Mashariki.

"Lengo la Tanzania kuwa na madaktari bingwa na miundombinu ya kutoa Huduma za kibingwa na bingwa bobezi ni kuhakikisha fedha ya kigeni haiendi nje ya nchi ili kusaidia kugharamia watanzania wasaio kuwa na uwezo wa kupata matibabu hapa nchinI", ameeleza Dkt. Mollel.

Naye Mkurugenzi mtendaji wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete(JKCI) Dkt. Peter Kisenge alisema kuwa madaktari hao watafanya upasuaji kwa watoto wenye umri chini ya miaka 15 na wanatarajia kufanya upasuaji kwa watoto 10.

"Mpaka sasa Zambia washapokea wagonjwa 15 wanaohitaji Huduma ya upasuaji wa moyo hivyo watalaalamu wetu watatoa Huduma kwa hao wagonjwa na wengine watakao hitajika kupata Huduma zaidi watapewa rufaa ya kuja nchini kupata matibabu zaidi", amesema Dkt. Kisenge

# Zingatieni maadili utu na heshima katika kutoa huduma za afya.

**Na. Said Nyaoza**
**Dodoma**

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. Grace Magembe amewataka wahudumu wa afya kuzingatia utoaji wa huduma bora kwa wananchi kupitia misingi ya maadili, utu na heshima ili kuendelea kuleta mabadiliko na maende yanayoendana na utoaji wa huduma.

Dkt. Magembe amesema hayo wakati akifungua kikao kazi cha kada za Madaktari na wauguzi kilichofanyika Mkoani Dodoma chenye lengo la kujadili namna ya kuboresha utoaji huduma bora wananchi.

Dkt. Magembe alisema utoaji wa huduma bora kwa wananchi utasaidia kuleta upendo na heshima hivyo kusababisha wananchi kufurahia huduma zinazotolewa kupitia vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

"Ndani ya miaka miwili ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amewezesha upatikanaji wa huduma za Afya karibu na wananchi kwa asilimia 70 kwa mijini na vijijini hivyo wananchi wanafikiwa na huduma za afya ndani ya km 5, hatuna tunachomdai Rais Maende na mafanikio kwenye Sekta ya Afya ni makubwa kinachotakiwa sasa hivi ni sisi watumishi kubadilisha fikra zetu na uwajibikaji wetu". Asema Dkt. Magembe.

Aidha, Dkt. Magembe alisema hakuna huduma bora bila mabadiliko ya watumishi katika kila kada ndani ya sekta ya afya hivyo ni lazima kuangalia kwa uhalisia kwani suala la kuhudumia wananchi kwa heshima, haki linaanzia getini wakati mgonjwa anaingia kufuata huduma.

Dkt. Magembe aliwashukuru wadau wa maende katika sekta ya afya kwa kushirikiana na Serikali na kuhakikisha wanafikisha huduma kwa makundi yote ya Wananchi.

Mwisho, Dkt. Magembe aliwahakikishia watanzania kutokanana na maboresho yote yaliyofanyika katika Sekta ya Afya muelekeo wa serikali ni kujikita zaidi kwenye ubora wa utoaji huduma ili ziendane na maboresho haya.






# Serikali kuimarisha hali ya lishe kwa vijana balehe nchini

**Na. Hassan Kimweri**
**Dar Es Salaam**

Serikali kupitia Wizara ya Afya imedhamiria kuimarisha na kuwekeza kwenye Afya za vijana balehe hasa katika hali za Lishe, Afya ya Akili pamoja na elimu ili kujikinga na magongwa yakuambukiza ikiwemo VVU/UKIMWI ikiwa ni kipaumbele cha Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amesema hayo wakati akifungua Kongamano la Tano la Kisayansi kuhusu masuala ya vijana balehe (15-19) lenye lengo la kujadili namna ya kubadili Tafiti za Afya kwa Vijana wa rika balehe na Lishe kuwa za vitendo.

“Vijana hawa balehe wana changamoto nyingi ikiwemo ya masuala ya lishe, Afya ya Uzazi, Afya ya Akili, lakini pia vijana wengi wanakabiliwa na upungufu wa damu kwa asilimia 38-40, uzito mkubwa, uzito mdogo pamoja na ukosefu wa vitamini.” Amesema Waziri Ummy

Waziri Ummy Mwalimu alisema, Kangamano hilo limekutanisha wanasayansi mbalimbali kutoka Afrika, Marekani na Ulaya ili kujadili kwa pamoja ni vipi Tanzania itaweza kutumia Tafiti za Kisayansi katika kufanya maamuzi ya kisera pamoja na masuala ya Afya ya Uzazi.

“Katika Kongamano hili pia tumeona kuzinduliwa kwa utafiti ambao umeonesha kwamba, endapo wakina mama wajawazito watapewa madini ya ‘calcium’ tunaweza tukapunguza kifafa cha mimba kinachochangia vifo vya kina mama wajawazito.” Amesema Waziri Ummy

Aidha Waziri Ummy alisema, utafiti huo umeonesha badala ya kuwapa dozi ya Mg 1,500 kwa siku hata wakipewa dozi ya Mg 500 kwa siku inaweza kusaidia matokeo mazuri kwa kinamama wajawazito kutopata kifafa cha mimba ambapo pia itapumguza vifo vya wajawazito na watoto wachanga.

Mwisho, Waziri Ummy alitoa wito kwa Watanzania ikiwemo vijana kuzingatia mtindo bora wa maisha ikiwemo ulaji kwa kupunguza mafuta, chumvi na Sukari pamoja na kufanya mazoezi ili kuepuka Magonjwa Yasiyoambukiza kwa kuwa vijana nao wanakabiliwa na magonjwa hayo.



# Kampeni ya taulo za kike milioni 5 kwa wanafunzi waliopo shuleni yazinduliwa.

**Na. Majid Abdulkarim**
**DODOMA**

Wizara ya Afya imepokea paketi 2,952 sawa na pedi 29,520 ikiwa ni ishara ya kuzindua rasmi Kampeni ya kuchangia pedi kwa wanafunzi ambazo zitagawiwa kwa wasichana waliopokatika shule za msingi na sekondari nchini.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi wa Huduma za Tiba Wizara ya Afya, Prof. Pascal Ruggajo wakati alipomwakilisha Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel wakati akipokea pedi zilizotolewa na Kampuni ya Mawasiliano ya Simu Halotel.

"Pedi hizi ambazo tumezipokea zitasambazwa kwenye shule za Mkoa wa Dodoma kwa kuanzia na pedi zitaendelea kugawiwa kwa wasichana waliopo shuleni kadri zinavyo patikana", ameeleza Prof. Ruggajo

Prof. Ruggajo alisema lengo la Kampeni hiyo ni kuchangisha paketi za pedi milioni 5 ambazo zitasambazwa kwenye shule ili kuhakikisha mtoto wakike anapata hedhi salama

Vile vile alitoa wito kwa wadau mbalimbali kujitokeza katika kampeni ya kuchangia pedi kwa wanafunzi ambazo zitagawiwa kwa wasichana waliopo katika shule za msingi na sekondari nchini ili kutatua changamoto ya upungufu wa pedi salama kwa matumizi ya wasichana na wanawake.

Alisisitiza kuwa elimu inahitajika zaidi kwa jamii ili kuona suala hilo ni Baraka na sio laana au mikosi kwani suala la hedhi limezungukwa na usiri mkubwa kiasi kwamba jamii inakosa fursa ya kujadili kwa uwazi namna ya kuliboresha kuanzia ngazi ya kaya hadi kwenye taasisi hivyo kuna ulazima wa jamii kwendelea kupatiwa elimu juu ya hedhi.

Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Jukwaa la Hedhi Salama imekuwa ikichukua hatua za kukabiliana na changamoto hizo ikiwa ni kuanzishwa kwa kampeni ya kuchangia pedi kwa wanafunzi yenye kauli mbiu ya Pedi Yangu Afya Yangu.





# Wananchi watakiwa kuchukua tahadhari kukabiliana na ugonjwa wa kipindupindu

**Na. Shaban Juma**
**Shinyanga**

Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu amewataka wananchi kuchukua tahadhari kwa kufanya usafi na kuzingatia matumizi sahihi ya vyoo Pamoja na kunywa maji safi na salama ili kuepukana na ugonjwa wa Kipindupindu.

Hayo ameyasema katika mkutano wa hadhara na wananchi wa Kata ya Igumilo Wilaya ya Kishapu Mkoani Shinyanga mara baada ya kukagua chanzo kinachosadikika kuwa chanzo cha ugonjwa huo ambao ni Mto Tungu.

"Niwaombe wananchi kuzingatia usafi na kwa mgonjwa yeyote yule ambao ana dalili za ugonjwa huu ikiwa ni kutapika na kuharisha basi awaishwe kwenye kituo cha afya na mtoe taarifa kwa viongozi ili hatua za haraka zichukuliwe". Amesema Prof. Nagu.

Aidha Prof. Nagu alisema kila wananchi anawajibu wa kulinda afya yake na familia yake kuwakinga na madhara Pamoja na mlipuko huu wa kipindupindu kwa kutumia maji safi na salama kwa kuyatibu na dawa au kuchemsha na kuhifadhi sehemu iliyo salama.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Mhe. Christina Mndeme amehimiza matumizi sahihi ya vyoo na kuwataka wananchi wote wazingatie usafi wa mazingira ili kuendelea kuudhibiti ugonjwa wa Kipindupindu usiendelee.

Mhe. Mndeme alisema ni wajibu wa kila mwananchi kuchukua tahadhari dhidi ya Ugonjwa wa Kipindupindu na kufuata ushauri wa wataalamu katika kukabiliana na ugonjwa huu.

Hata hivyo amewataka watendaji wa kata kuhakikisha wananchi wote wanatumia vyoo na yule atakaebainika hana choo katika kaya yake awajibishwe kisheria.






# Undeni miongozo inayotekelezeka ili iwajenge uwezo watumishi na wanafunzi vyuo vya afya

**Na. Said Nyaoza**
**Morogoro**

Mkurugenzi wa Huduma za Uuguzi na Ukunga katika Wizara ya Afya, Bi. Ziada J. Sellah, alisisitiza umuhimu wa kuundwa kwa miongozo inayotekelezeka kwa ufanisi ili kujenga uwezo wa watumishi na wanafunzi wa vyuo vya afya kwa lengo la kuhakikisha huduma bora zinatolewa kwa wananchi.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha kupitia kitita cha mafunzo kwa wakufunzi kwa vitendo Mkoani Morogoro, Bi. Ziada alieleza kuwa baadhi ya wahitimu hawana uwezo wa kutosha wanapofika kazini. Hivyo, amesisitiza umuhimu wa kupeleka wakufunzi kwa vitendo kuanzia ngazi ya vyuo hadi vituo vya huduma za afya ili kujenga uwezo wao.

Aidha, alisisitiza kuwa mafunzo yanapaswa kugusa kada zote katika sekta ya afya, kutoka kwa watumishi wa juu mpaka wale wa chini, kama vile walinzi. Hii ni kwa sababu kila mtu katika mfumo wa afya ana jukumu muhimu katika kutoa huduma bora kwa wagonjwa.

"Mhe. Waziri na Katibu mkuu walisema hatuwezi kuishia kwa wauguzi tu kuwajengea uwezo ni vyema tushuke hadi chini kwa mlinzi kwa sababu yeye ndo mtu wa kwanza kumpokea mgonjwa getini, hivyo hii miongozo ilenge kuwagusa kada zote" amesema Bi. Ziada.

Bi. Ziada alihimiza pia kufanyika kwa mafunzo ya utangulizi kwa wafanyakazi wapya wanapoanza kazi ili kuhakikisha wanakumbushwa miongozo ya kazi kwani itasaidia kuhakikisha kuwa watumishi wanaoingia kazini wanafahamu na kuzingatia miongozo inayohitajika katika kutoa huduma za afya.

Bi. Ziada alisisitiza umuhimu wa kuweka mkazo katika mafunzo ya mara kwa mara ili kuhakikisha watumishi wa afya wanabaki katika kiwango cha juu cha utendaji na kusema kuwa mafunzo hayo yanapaswa kuwa ya ubunifu na kuzingatia mabadiliko ya haraka katika sekta ya afya.

Mwisho Bi. Ziada alitoa wito kwa wadau wote katika sekta ya Afya kushirikiana kwa karibu ili kuhakikisha kuwa miongozo inayoundwa inatekelezwa kikamilifu na kwa ufanisi kwani itasaidia kufikia lengo la kutoa huduma bora za afya kwa wananchi wote.




# Mwaka 2023 wagonjwa 15,386 wamepata huduma mpya za CT - SCAN hospitali za rufaa za mikoa

**Na Englibert Kayombo,**
**Dar Es Salaam**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu alisema katika mwaka 2023 wagonjwa 15,386 walipata huduma za CT - Scan katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ambapo hapo awali huduma hiyo ilikuwa haipatikani katika Hospitali hizo.

Waziri Ummy Mwalimu alisema hayo wakati akitoa taarifa ya hali ya utoaji huduma za Afya nchini kwa mwaka 2023 katika mkutano wake na Waandishi wa habari uliofanyika katika ofisi ndogo za Wizara ya Afya Jijini Dar es salaam.

“Uwekezaji huu umeleta mabadiliko makubwa katika huduma za uchunguzi wa magonjwa na hivyo kupelekea huduma hizi kuwafikia wananchi kwa urahisi katika maeneo wanayoishi na kupunguza usumbufu wa kupoteza muda na gharama za kupata matibabu.” Alisema Waziri Ummy

Aidha, Waziri Ummy wakati akiendelea kuelezea mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Afya Mwaka 2023 alisema mashine ya kuchunguza magonjwa kama ya misuli, mishipa ya damu na fahamu, ubongo na vivimbe (MRI) zimeongezeka kufikia 13 ambapo awali (Mwaka 2022) zilikua Sita.

“Lakini pia, mashine ya kuchunguza magonjwa ya misuli, ubongo, viungo vya mwili (CT SCAN) zimeongezeka kufikia 45 Mwaka 2023 ambapo awali zilikua 22 tu.” Alisema Waziri Ummy

Alisema, pamoja na mashine za Digital X- Ray zimeongezeka kufikia 346 na zote zinafanya kazi ambapo kwa Mwaka 2022 zilikua mashine 296 pamoja na mashine za Utra Sound, Disemba 2022 zilikuwa 192 huku Disemba 2023 zimefikia 512 ongezeko la mashine 320.



# Simamieni usafi katika maeneo yenu (kipindupindu kinaletwa na uchafu)

**Na. Shaban Juma**
**Mwanza**

Watendaji wa kata na mwenyeviti wa mitaa wametakiwa kusimamia usafi katika maeneo yao ili kuendelea kuudhibiti ugonjwa wa Kipindupindu nchini.

Kauli hiyo imetolewa na Mganga mkuu wa serikali Prof Tumaini Nagu katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza kwenye ofisi za mkuu wa wilaya Mhe. Amina Makilagi wakati wa kikao na watendaji wa Kata juu ya kutokomeza ugonjwa wa Kipindupindu katika Jiji hilo.

Prof. Nagu aliwaomba watendaji kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha Usafi wa mazingira katika makazi ya wananchi kwa kusimamia kwani ugonjwa huu unasababishwa na Uchafu.
“Kipindupindu kinaletwa na uchafu, hivyo maeneo yetu lazima tuyalinde kwa kufanya usafi bila ya usafi ugonjwa huu utawaathiri wengi. Njia pekee ya kuudhibiti ni kuwa wasafi katika maeneo yetu”. Alisema Prof. Nagu

Sambamba na hilo Prof. Nagu alisisitiza unawaji wa mikono kwa kutumia maji safi na salama pamoja na kunywa maji yaliy ochemshwa au kutibiwa kwa dawa ambazo zinatolewa bure na serikali.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana Mhe. Amina Makilagi alielezea mikakati ya kuhakikisha ugonjwa wa Kipindupindu unadhibitiwa katika Halmashauri yake ikiwa ni Pamoja na kuendelea kuwatumia watendaji na mwenyeviti katika kutoa elimu kwa wananchi juu ya kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa Kipindupindu.

Hali ya ugonjwa wa Kipindupindu imeendelea kuimarika katika mkoa wa Mwanza kutokana na juhudi za serikali katika kuwekeza nguvu kwenye kuudhibiti ugonjwa huu kwa kutoa Vifaa tiba, Vifaa kinga na dawa.



# Vituo vipya 485 vya kutoa huduma za afya vimeongezeka kwa mwaka 2023

**Na. Aisha Swahibu,**
**Dar Es Salaam,**

Vituo vipya 485 vya kutolea huduma za Afya vimeongezeka kutoka vituo 8,881 Disemba 2022 na kufikia vituo 9,366 Disemba 2023 sawa na ongezeko la asilimia 5.5 ikiwa ni mafanikio makubwa katika Sekta ya Afya.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amesema hayo wakati akitoa taarifa ya hali ya utoaji huduma za Afya nchini kwa mwaka 2023 katika mkutano wake na Waandishi wa habari uliofanyika katika ofisi ndogo za Wizara ya Afya Jijini Dar es salaam.

Amesema, Mgawanyo wa vituo hivyo vipya vya kutoa huduma za Afya hadi kufikia Disemba 2023 ni pamoja na Zahanati – 7,804 (83.3%), Vituo vya Afya – 1,126 (12.02%), Hospitali za Halmashauri – 171 (1.83%), Hospitali zenye hadhi ya Wilaya -180 (1.92%).

Pia, Hospitali za Rufaa za Mikoa – 28 (1.3%), Hospitali zenye hadhi ya Mkoa- 34 (0.36%), Hospitali za Rufaa za Kanda – 5 (0.05%), Hospitali zenye hadhi ya kanda- 11 (0.12%), Hospitali Maalumu – 6 (0.06%), Hospitali ya Taifa – 1 (0.01%).

"Ongezeko la vituo vya kutoa huduma za afya nchini limetuwezesha kusogeza huduma za Afya karibu zaidi na wananchi kama tunavyoelekezwa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025." Amesema








# Wizara ya afya yatoa elimu kwa wanahabari juu ya ukoma

**Na. Emmanuel Malegi,**
**Dodoma**

Katika kuelekea maadhimisho ya siku ya Ukoma dunia Serikali kupita Wizara ya Afya imetoa elimu juu ya kuthibiti ugonjwa wa Ukoma kwa Waandishi wa Habari.

Elimu hiyo iliutolewa tarehe 27 Januari, 2024 Dodoma na Mratibu wa mpango wa Taifa wa kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma Wizara ya Afya Dkt. Deusi Kamara wakati wa akizungumza na waandishi wa habari.

Dkt. Kamara alisema ugonjwa wa Ukoma unasababishwa na bakteria aitwae Mycobacterium Leprae na unaambukizwa kwa njia ya hewa hivyo jamii kuacha dhana potofu juu ya ugonjwa huo.

"Vimelea vya ugonjwa wa ukoma vinaambukiza kwa njia ya hewa, endapo mtu mwenye vimelea vya ugonjwa huu akakohoa au kupiga chafya bila kuziba mdomo basi anaweza kumuambukiza mtu mwingine ivyo tuachane na dhana potofu za kusema mtu mwenye ugonjwa huu analaana au amerogwa" Amesema Dkt. Kamara.

Alisema dalili za ugonjwa wa Ukoma ni mtu kupata mabaka yenye rangi ya shaba ambayo hayawasi wala kuuma na kuvimba kwa mishipa ya fahamu kwa sababu ya vimelea vya ugonjwa huo kupenda kuzalia kwenye mishipa ya fahamu.

"nitoe wito kwa jamii pindi unapoona dalili kama hizi au mabadiliko yoyote kwenye ngozi yako, kama ni mabaka, vipele au uvimbe ni vyema kuwahi katika kituo cha kutolea huduma za Afya ili unapogundulika umepata maambukizi ya ugonjwa huu kuanza tiba mara moja kwa sababu ukoma unatibika na tiba zake kutolewa bure kwenye vituo vya Afya kote nchini". Amesema

Pia Dkt. Kamara aliwataka waandishi wa habari kutumia vizuri vipawa vyao katika kusambaza elimu na hamasa kwa jamii dhidi ya mapambano ya kutokomeza unyanyapaa dhidi ya waathirika wa ukoma.

Ugonjwa wa Ukoma uadhimishwa kila ifikapo tarehe 28 Januari ya kila mwaka Duniani ambapo kitaifa mwaka huu yanakwenda na kauli mbiu "Thamini Utu; Tokomeza Unyanyapaa dhidi ya Waathirika wa Ukoma



# Wananchi chukueni tahadhari dhidi ya red eyes

**Na Shaban Juma**
**Dodoma**

Wizara ya afya imewaasa wananchi kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa macho mekundu (Red eyes) Maambukizi ya Kirusi kwenye ngozi ya juu ya gololi ya jicho yajulikanayo kitaalamu "Viral Keratoconjunctivitis" iliyoibuka nchini hivi karibuni.

Hayo yamesemwa  na Mkurugenzi wa Huduma za Tiba Wizara ya Afya Prof Pascal Ruggajo kwa niaba ya Mganga Mkuu wa Serikali Prof Tumaini Nagu wakati akitoa taarifa ya uchunguzi wa awali ya ugonjwa huo ambao umeripotiwa kuathiri watu wengi nchini.

Prof. Ruggajo alisema dalili ya ugonjwa huo ni pamoja na macho kuwasha, kuchomachoma, kuuma, macho kutoa machozi na kutoa tongo tongo za njano.

"Taarifa za uchunguzi zinaonesha Maambukizi ya Kirusi hiki kwenye ngozi ya juu ya gololi ya jicho yajulikanayo kitaalamu "Viral Keratoconjunctivitis" ni maambukizi yanayosambaa kwa kasi kubwa. Hakuna tiba maalumu kwa ugonjwa huu na hata bila tiba dalili huisha zenyewe ndani ya wiki mbili". Amesema Prof Ruggajo.

Prof. Ruggajo alisema mwenendo wa ugonjwa huo unaonyesha kuna ongezeko kubwa la wagonjwa wanaofika katika Vituo vya kutolea huduma za afya wakiwa wanasumbuliwa na ugonjwa huo.

"Katika kipindi cha Desembe 22, 2023 hadi kumekuwa na ongezeko kubwa la watu wanaosumbuliwa na ugonjwa huu kufika katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa ajili ya matibabu, kwa mfano katika mkoa wa Dar Es Salaam kuna wagonjwa wapya 869 huku hali ya kawaida katika kipindi cha mwezi Desemba 2023 kulikuwa na wagonjwa 17 pekee" alifafanua Prof. Ruggajo.

Aidha alisisitiza suala la usafi ni jambo muhimu katika kuzuia maambukizi kusambaa kwa wengine Kutokana na tabia ya ugonjwa huu kusambaa kwa kasi, maambukizi haya huleta mlipuko ambao husambaa kupitia kirusi kwa asilimia zaidi ya 80%.

Prof Ruggajo amewashauri wananchi kutokutumia dawa zisizo rasmi na ambazo hazijaandikwa na daktari kwa wakati huo na kutotumia dawa za macho anazotumia mgonjwa mwingine ili kuepuka madhara kwa kuwa dawa za macho ni tofauti na kwa matumizi tofauti.

# Sekta ya afya kuendelea kuweka kipaumbele ajenda ya kupunguza vifo vya mama na mtoto



**Na. Aisha Swahibu,**
**Dodoma**

Sekta ya Afya kuendelea kuweka kipaumbele ajenda ya kupunguza vifo vya mama na mtoto katika vikao vinavyofanyika ngazi zote za Mkoa ili kuendelea kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi ikiwa ni malengo ya Taifa na Dunia.

Hayo yamesemwa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule Jijini Dodoma wakati akifungua kikao kazi chenye lengo la kujadili mikakati ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, mama na watoto.

"Kupunguza vifo vya mama na mtoto ni malengo ya Dunia lakini pia Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni dhamira yake hivyo sisi watendaji wake ni lazima tupambane nayo kwa kumuunga mkono Rais na Dunia kwa ujumla." Amesema Mh. Senyamule.

Amesema, ni vyema Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Kijiji awe anashiriki vikao vya kikanuni katika ngazi zote za Halmashauri ili aweze kutoa taarifa ya hali ilivyo juu ya vifo vinavyotokea pamoja na changamoto zake.

Aidha, Mhe. Senyamule alitoa wito kwa Waganga Wakuu wa Wilaya kupeleka taarifa za Wilaya juu ya vifo vya mama na mtoto kila wiki katika ofisi za Wakuu wa Wilaya ili kuwa na mkakati wa pamoja wa kuondoa vifo visivyo na ulazima kwa kushirikiana na wataalamu.

Katika hatua nyingine, Mhe. Senyamule alisema Serikali imedhamiria kupunguza tatizo la Kansa ya Uzazi kwa wanawake hivyo amewahimiza akinamama kujitokeza kupima ili waweze kupata matibabu haraka kwa kuwa huduma hiyo inatolewa bila malipo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Idara ya Afya ya Uzazi Mama na Mtoto, Dkt. Ahmad Makuwani alisema Wizara ya Afya imeongeza kiwango cha watumiaji wa Vituo vya Afya wakati wa kujifungua na kufikia asilimia 81 ambapo 2016 tulikuwa na asilimia 63.

"Hii ina maana kwamba katika kila wajawazito 10, wajawazito 8 wanajifungulia katika Vituo vya kutolea huduma za Afya hivyo tumepunguza vifo vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 556 katika kila vizazi hai Laki Moja hadi vifo 104 katika kila vizazi hali Laki Moja ambavyo vimepungua kwa asilimia 80". Amesema Dkt. Makuwani.



# Rc Homera aipongeza wizara ya afya kwa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi

**Na. Emmanuel Malegi, Mbeya**

Serikali kupitia Wizara ya Afya imepongezwa kwa juhudi kubwa inayoendelea kufanya za kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, mama na mtoto ikiwa ni kipaumbele cha Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Pongezi hizo zimetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Mhe. Juma Homera wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha kujadili mikakati ya kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi, mama na mtoto.

"Vifo vitokanavyo na uzazi, mama na mtoto vimeendelea kupungua nchini, pongezi kwa Wizara ya Afya kwa kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan kwa vitendo." Amesema Mhe. Homera


Alisema, Rais Dkt. Samia amefanya kazi kubwa ya kutafuta fedha za ujenzi wa jengo la kuhudumia mama na mtotokatika Hospitali ya Kanda ya Mbeya (META) na ununuzi wa vifaa vya kisasa.

"Kwa uwekezaji huu unaofanywa na Serikali ya Rais Samia ni lazima watumishi kuwa waadilifu na wazalendo kwa kufanya kazi kwa kuzingatia maadili ya kazi, Taaluma na weledi." Amesema Mhe. Homera

Aidha, Mhe. Homera alisema ili kunaondokana na changamoto ya upatikanaji wa damu salama ni lazima kuwe na mikakati ya pamoja kwa Mikoa ya nyanda za juu Kusini Magharibi kwa kuchangia damu salama.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Dkt. Elizabeth Nyema amewataka watumishi wa Sekta ya Afya kuwajibika na kuzidisha ushirikiano ili kwa pamoja kuendelea kupunguza vifo visivyo vya lazima vinavyotokana na Uzazi, mama na mtoto.

Kikao hicho chenye kauli mbiu ya 'Uongozi na uwajibikaji ni chachu ya punguza vifo vitokanavyo na Uzazi, mama na mtoto' kimehusisha watumishi kutoka Sekta ya Afya wa kanda ya nyanda za juu Kusini Magharibi kutoka Mkoa mwenyeji wa Mbeya, Songwe na Rukwa.



# Zaidi ya asilimia 74 ya watanzania wanapata huduma za afya ngazi ya msingi

**Na Said Nyaoza,**
**Dar Es Salaam**

Serikali kupitia Wizara ya Afya imeendelea kuboresha huduma za Afya ambapo kwa Mwaka 2023 zaidi ya asilimia 74 ya Watanzania wamepata huduma za Afya katika ngazi ya msingi (Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya pamoja na Halmashauri).

Waziri Ummy Mwalimu alisema hayo wakati akitoa taarifa ya hali ya utoaji huduma za Afya nchini kwa mwaka 2023 katika mkutano wake na Waandishi wa habari uliofanyika katika ofisi ndogo za Wizara ya Afya Jijini Dar es salaam.

“Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais TAMISEMI itaendelea kuongeza nguvu ya kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa utoaji wa huduma za Afya ngazi ya msingi ili Watanzania wengi wapate huduma bora zilizopo karibu nao.” Alisema Waziri Ummy

Waziri Ummy alisema kwa Mwaka 2023 mahudhurio ya wagonjwa wa nje (OPD) imeongezeka na kufikia Mil. 42,252,741 kutoka wagonjwa 41,347,690 kwa mwaka 2022.

“Katika mwaka 2023, Wagonjwa hawa wamepata huduma katika ngazi za Zahanati kwa 33%, Kituo cha Afya - 18%, Hospitali za Halmashauri - 23%, Hospitali za Rufaa za Mikoa – 9%, Hospitali za Rufaa za Kanda, Maalum na Taifa – 17%.” Alisema Waziri Ummy

Ameongeza kuwa Wagonjwa waliopata huduma ya Kulazwa (IPD) kwa Mwaka 2022 ni wagonjwa Mil. 1,630,722 na Mwaka 2023 kulikuwa na wagonjwa Mil. 1,622,979.

“Mwaka 2023, wagonjwa hawa wamepata huduma katika ngazi za Kituo cha Afya - 26%, Hospitali za Halmashauri – 51%, Hospitali za Rufaa za Mikoa – 13%, Hospitali za Rufaa za Kanda, Maalum na Taifa – 10%.” Alisema Waziri Ummy







# Tanzania na wana-diaspora kuendelea kushirikiana kuboresha huduma za afya nchini

**Na. Cletus Sangas,**
**Dar es Salaam**

Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan kupitia Wizara ya Afya iko tayari kuzidisha mashirikiano na Wana-Diaspora ili kuendelea kuboresha upatikanaji wa Huduma za Afya kwa Watanzania.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu alisema hayo wakati wa mkutano wake na Watanzania wanaofanya kazi katika Sekta ya Afya nchini Uingereza uliofanyika kwa njia ya mtandao.

Waziri Ummy alisema lazima kuwepo na dawati maalumu litakaloratibu mawasiliano na uhusiano baina ya Wizara ya Afya na Diaspora ambalo litakuwa chini ya Mganga Mkuu wa Serikali.

"Tunahitaji kuangalia namna gani tunaweza kuvutia wadau ambao wako tayari kufanya uwekezaji nchini katika kuongeza vituo vya kutoa huduma za Afya pamoja na maabara zitakazoweza kufanya vipimo maalumu. Alisema Waziri Ummy.

Alisema, Serikali imepiga hatua kubwa katika kuhakikisha huduma za Afya zinasogezwa karibu zaidi na wananchi kwa kufanya maboresho ya ujenzi wa Hospitali katika ngazi mbalimbali, upatikanaji wa Vifaa pamoja na Vifaa Tiba vya kisasa.

"Tunamshukuru sana Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa tutupatia Tsh. Bilioni 8 kwa jili ya kupeleka wataalam kwenda kupata mafunzo nje ya nchi kwa Seti na sio mmoja mmoja kama ilivyokuwa awali." Alisema Waziri Ummy

Mwisho, Waziri Ummy aliwashukuru na kuwapongeza Wana-Diaspora kwa kazi nzuri wanazozifanya kwa kushiriana na Hospitali zilizopo nchini Tanzania ikiwemo Hospitali ya Tumbi, Hospitali ya Mnazi mmoja pamoja na MOI.

# Msd yaanza kusambaza vifaa tiba vya huduma za afya ya uzazi katika majimbo 214 nchini.

**Na. Emmanuel Malegi,**
**Dar Es Salaam**

Bohari ya Dawa (MSD) imeanza kutekeleza agizo la Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu la kusambaza vifaatiba vya Huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto katika Majimbo yote 214 Tanzania bara.

Mnamo Waziri Ummy Mwalimu akiwa anapokea vifaatiba hivyo Jijini Dar Es Salaam alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imefanikisha ununuzi wa Vifaatiba hivyo vilivyogharimu kiasi cha Shilingi Bilioni 14.9 kwa ajili ya kuboresha huduma za afya ya uzazi mama na mtoto nchini na kuiagiza MSD kuanza haraka kazi ya usambazaji wa vifaatiba hivyo.

Akipokea vifaatiba hivyo Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mhe. Adam Malima,alisema Serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika miundombonu ya Sekta ya Afya na kwa sasa imejielekeza katika uboreshaji wa viwango vya utoaji wa huduma za afya nchini.

“Malengo yetu sisi Mkoa baada ya kupokea kwa vifaa tiba hivi ni kwenda kuboresha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi na hili tumekuwa tukilihimiza nyakati zote” Amesema Mhe. Malima .

Mhe. Malima aemesema licha ya kupokea vifaa tiba hivyo, mkakati wa Mkoa ni kuendelea kutoa elimu kuhusiana na kujikunga na magonjwa mbalimbali na namna ya utumiaji wa vifaa hivyo kwa wagonjwa.

Kwa upande wake Meneja wa MSD, Kanda ya Mashariki yenye Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani ,Morogoro na Visiwani Zanzibar, Betia Kaema alisema hayo wakati wa makabidhiano wa vifaa hivyo na mkuu wa mkoa wa Morogoro , Adam Malima kwa ajili ya majimbo 11 ya mkoa huo.

Kaema alisema , Mkoa wa Morogoro umepata vifaa aina tisa vyenye thamani ya Shilingi Milioni 759 na kuanza kusambazwa katika majimbo yote 11 na kila jimbo litapokea vifaa vyenye thamani ya Shilingi Milioni 69.

Kaema alivitaja vifaa vilivyokabidhiwa kwa kila jimbo la mkoa huo ni Drip stand (330), vitanda vya kawaida vya wagonjwa (330), vitanda vya kujifungulia mama wanajawazito (220) na seti (220) za kujifungulia mama wajawazito, shuka (1,320), magodoro (330), Examination table (220), meza ndogo za wagonjwa kuwekea vifaa vyao pale wanapokuwa wamelazwa (165) na Bed side Locker (330).





# Wagonjwa 6,931 kutoka nje ya nchi walitibiwa Tanzania, mwaka 2023

**Na Hassan Kimweri,**
**Dar es Salaam**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amesema Mwaka 2023 Tanzania iliweza kuvutia Wagonjwa 6,931 kutoka nje ya Nchi kufika nchini kwa ajili ya kupata huduma za matibabu katika Hospitali sita hapa nchini.

Waziri Ummy amebainisha hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari Jijini Dar Es Salaam akiwasilisha taarifa ya hali ya utoaji huduma za afya nchini kwa mwaka 2023 na vipaumbele vya Sekya ya Afya Mwaka 2024.



Waziri Ummy alisema kwa mwaka 2022 idadi ya wagonjwa kutoka nje ya nchi waliofika nchini Tanzania kwa ajili ya matibabu ilikuwa ni 5,705 hivyo kufanya idadi hiyo kuongezeka kwa asilimia 121 hadi kufikia wagonjwa 6931 mwaka 2023.

Amebainisha kuwa uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye kuboresha huduma za kibigwa na bobezi katika sekta ya afya umesaidia kuvutia nchi jirani kufata Huduma za afya nchini.

Waziri Ummy amesema kuwa Wagonjwa hao wanatoka katika Nchi za Comoro, Malawi, Burundi, Zambia, Congo DRC, Uganda, Zimbabwe na Kenya ambapo walihudumiwa katika Hospitali sita ikiwemo Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Taasisi ya Mifupa MOI, Hospitali ya Agha khan na Hospitali ya Saifee.

# Tanzania yapiga hatua katika kukabiliana na majanga na Dharura za Kiafya

**Na. Majid Abdulkarim**
**Tanga**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amezitaka Hoslitali zote za Umma kutekeleza kwa ukamilifu maelekezo yaliyokwisha tolewa na Serikali ya Marufuku Hospitali kuzuia miili ya marehemu kwa kigezo cha kushindwa kulipa deni la gharama za Matibabu.

Waziri Ummy ametoa agizo hilo wakati akijibu swali la katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi Paul Makonda katika mkutano wa hadhara uliofanyika jijini Tanga Januari 20, 2024. lililouliza ni upi mkakati wa Serikali wa kuwasaidia wananchi maskini wanaoshindwa kulipia gharama za matibabu kwa kudaiwa kulipia maiti ili hali hawana Uwezo wa kilipa deni na kukomboa mwili.

Naomba nitumie mkutano huu kuzitaka hospitali zote za serikali, marufuku kuzuia maiti ya mtanzania wowote, haya ndio maelekezo ya Serikali, nawataka Waganga Wafawidhi wa Hospitali zote za Serikali nchini kuzingatia muongozo wa Serikali wa kutozuia maiti, tafuteni njia nyingine, toeni maiti wakizika mtakuja kudaiana mambo mengine" alisema Waziri Ummy.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu alitoa rai kwa viongozi wa Mikoa na Wilaya nchini kote kutosita kuwachukulia hatua kwa baadhi ya watendaji na watoa huduma za afya ambao watakiuka maadili, miiko, Miongozo na melekezo ya serikali katika kutoa huduma za Afya.

"Tunataka kuhakikisha watendaji wa wilaya na mikoa wanawajibika kwa utoaji wa huduma za afya katika maeneo yao, kauli yangu ni kwa watumishi wa afya ambao wanakwenda kinyume na miongozo na maelekezo ya serikali wachukuliwe hatua mara moja na viongozi wa Wilaya na Mikoa pale ambapo watabainika kufanya uzembe" amesema Waziri Ummy.



# Lishe ni ajenda ya rais samia na bado ni kipaumbele katika sekta ya afya

**Na Hassan Kimweri**
**Dar Es Salaam**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amesema kuwa Suala la Lishe ni jambo kubwa ambalo limepewa kipaumbele katika Sekta ya Afya kwa kuwa ni ajenda kubwa ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Waziri Ummy Mwalimu alisema hayo alipokutana na watumishi wa Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC) baada ya kutolewa tamko la kufutwa kwa Taasisi hiyo na Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina.

"Ajenda hii ya lishe ni ajenda muhimu sana kwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan hii ni ajenda yake ambayo anaipa kipaumbele cha juu na sisi kama Wizara ni kipaumbele chetu." Alisema Waziri Ummy

Aidha, Waziri Ummy alisema hakuna mtumishi yoyote wa Taasisi hiyo atakae poteza haki zake na stahiki zake za msingi ikiwemo kazi na stahiki nyinginezo.

"Kazi kubwa tunayoifanya sasa ni kujadiliana namna bora zaidi ya kuendelea kusimamia masuala ya Lishe ndani ya Wizara na pia ndani ya Serikali kwa ujumla. Waziri Ummy alieleza kuwa kwa sasa jina la TFNC litaendelea kutumika hadi itakavyoelekezwa vinginenyo, kinachobadilika hapo ni hali ya kisheria 'legal status'".

Mwisho, Waziri Ummy alisema kuwa kazi na majukumu ya Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC) yataendelea kama kawaida kwa kutumia bajeti yao ya mwaka wa fedha 2023/2024.

Waziri Ummy ameambatana na timu kutoka Wizara ya Afya akiwemo Katibu Mkuu Dkt. John Jingu, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Grace Magembe pamoja na Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu.



# Watumishi simamieni sheria ndogo ndogo za Serikali za mitaa ili kukabiliana na kipindupindu

**Na. Abdulwaheed Madenge,**
**Mwanza**

Watumishi Sekta ya Afya wametakiwa kuhakikisha wanasimamia vyema sheria ndogondogo za serikali za mitaa katika kukabiliana na Ugonjwa wa Kipindupindu ili kuhakikisha afya ya jamii inaimarishwa na kuzingatiwa.

Hayo yamesemwa Mkoani Mwanza na Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu wakati wa kikao na Watumishi na wadau sekta ya Afya katika kujadili juhudi na mikakati ya kukabiliana na ugonjwa huo.

"Niwasisitize viongozi wenzangu juu ya dhamana tuliyopewa ya kuhakikisha Afya za watu zinaimarika vyema, hivyo ni wajibu wetu kuweza kusimamia misingi na mikakati tuliyoweka katika kuhakikisha wananchi wanakua salama". Amesema Prof. Nagu.

Aidha Prof. Nagu alisisitiza unawaji wa mikono kwa kutumia maji tiririka yaliyo safi na Salama Pamoja na kuzingatia hali ya usafi katika maeneo yenye mkusanyiko wa watu.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. Amoss Makalla amewataka wafanyabiashara wote kuzingatia kanuni za Afya katika maeneo yao ya biashara ili kuweza kuudhibiti ugonjwa huu.

Pia, Mhe. Makalla amelitaka Shirika linaloshughulikia masuala ya Barabara Vijijini na Mijini kuongeza kasi ya kusafisha mitaro na kuwakinga watumishi wanaosafisha mitaro kwa kuwapatia vifaa wezeshi kwa ajili ya kusafisha mitaro na kuondoa maji yaliyotuama.

Serikali imeendelea kufanya juhudi za kukabiliana na Ugonjwa wa Kipindupindu katika mikoa ya Mwanza na Shinyanga kwa kupeleka Vifaa tiba na Dawa ya kutibu maji takriban million saba ili kuendelea kuudhibiti ugonjwa wa Kipindupindu nchini.





# Wizara ya afya yaongeza kasi katika mapambano dhidi ya magonjwa yasiyopewa kipaumbele

**Na. Said Nyaoza,**
**Dar Es Salaam**

SERIKALI kupitia Wizara ya Afya imeongeza kasi ya kutoa elimu na dawakinga kwa jamii ili kuyatokomeza magonjwa yasiyopewa kipaumbele ifikapo 2030.

Yameelezwa hayo na Afisa Programu kutoka Mpango wa Taifa wa magonjwa yasiyopewa kipaumbele Wizara ya Afya Dkt. Isaac Njau katika semina ya waandishi wa habari Jijini Dar es Salaam.

Amesema mafunzo hayo ni sehemu ya maandalizi kuelekea Maadhimisho ya Siku ya Magonjwa yasiyopewa Kipaumbele Duniani (matende na mabusha, Usubi, Trakoma, Kichocho na Minyoo ya tumbo) inayotarajiwa kufanyika Januari 30, mwaka huu.

“Mwaka huu tumejipanga kuadhimisha Siku ya Magonjwa yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele, maadhimisho yatafanyika ngazi za mikoa na halmashauri kwa kutoa elimu na hamasa juu ya magonjwa haya katika jamii." Amesema.

Dkt. Clara Mwansasu ni Afisa kutoka Mpango huo wa kutokomeza magonjwa yasiyopewa kipaumbele alieleza kuwa, Tanzania imekuwa ikitekeleza afua za kutokomeza magonjwa hayo ikiwemo kutoa elimu na kumezesha dawa (NTD’s) baada ya kuwa imefanya tathmini ya kina.

Sambamba na hilo, alitoa wito kwa wananchi kuendelea kushiriki katika utekelezaji wa afua nyinginezo ikiwemo usafi wa mazingira na mwili kwani ni moja ya visababishi vikubwa vya magonjwa yasiyopewa kipaumbele.



# Watumishi sekta ya afya wametakiwa kuendelea kufuata miongozo ya kiutumishi

**Na. Eglibert Kayombo**
**Njombe**

Mkurugenzi Msaidizi wa Rasilimali Watu, Wizara ya Afya Bw. Danny Temba amewataka watumishi sekta ya Afya kuendelea kufuata miongozo na sheria za Kiutumishi iliyowekwa na Serikali kupitia Wizara ya Afya, kwa kuwa Serikali imewajengea miundombinu bora ya ufanyaji kazi.

Bw. Temba aliyasema hayo Mkoani Njombe katika hafla ya makabidhiano ya Ofisi kati ya aliyekuwa Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Njombe Dkt. Winfred Kyambile na Mganga Mfawidhi wa sasa Dkt. Gilbert Kwesi.

"Hospitali hii ni moja wapo wa hospitali nzuri yenye majengo na mazingira mazuri na yanatia moyo kufanya kazi, mnapaswa kujivunia kwa kufanya kazi katika mazingira mazuri kama haya hivyo mfuate miongozo ya kiutumishi iliyowekwa. Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassani amefanya kazi kubwa sana, hivyo tusimwangushe". Amesema Bw. Temba.

Pia aliwataka Viongozi wa Hospitali hiyo kusimamia vyema na kutumia mapato ipasavyo na kwa kufuata taratibu za kiserikali, lakini pia kutengeneza mazingira ya kufikiwa na watumishi na wananchi ili kutatua matatizo haraka.

Aidha Bw. Temba alimpongeza aliyekuwa Mganga Mfawidhi, Dkt. Winfred Kyambile kwa kazi kubwa ya usimamizi mzuri wa ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe pamoja na watumishi wote kwa kuwa sehemu ya mafanikio hayo .

"Rasmi kwa niaba ya Wizara, ya Afya tunampongeza Dkt. Kyambile kwa kazi nzuri aliyoi fanya ya kusimamia vyema ujenzi wa Hospital lakini pia tunatambua pia mchango mkubwa wa watumishi katika ujenzi huo." Amesema.

Naye aliyekuwa Mganga Mfawidhi Dkt. Winfred Kyambile, amewaomba watumishi kuendelea kufanya kazi kwa bidii na kutoa ushirikiano mkubwa kwa Mganga Mfawidhi, Dkt. Gilbert Kwesi.

Kwa upande wake Mganga Mfawidhi, Hospitali ya Rufaa mkoa wa Njombe, Dkt. Gilbert Kwesi, aliishukuru Serikali kupitia Wizara ya Afya kwa kumwamini, na kuahidi kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuzidi kuboresha utoaji huduma za Afya kwa wananchi.





# Muhimbili: Madaktari wazawa watenganisha watoto mapacha walioungana

**Na. Aisha Swahibu,**
**Dar Es Salaam**

Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa mara nyingine imeandika historia kwa kufanya upasuaji mkubwa wa kuwatengenisha watoto mapacha waliokuwa wameungana sehemu ya tumbo na kifua na kuwa upasuaji wa kwanza kufanywa na madaktari wazawa hapa nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa Huduma za Upasuaji Dkt. Rachel Mhaville alisema upasuaji huo umefanikiwa kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita kwa kununua vifaa tiba vya kisasa pamoja na kuwasomesha wataalamu.

“Tunachojivunia katika upasuaji huu ni kuwa umefanywa na timu ya madaktari wazawa, umefanyika kwa mafaniko makubwa na watoto wanaendelea vizuri kabisa. Lakini pamoja na kufanikiwa kufanya upasuaji huu bado tutaendelea kushirikiana na wataalamu wengine kwa ajili ya kuendelea kupata ujuzi zaidi na kuendeleza uhusiano” amesisitiza Dkt. Mhavile.

Kwa upande wake Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Watoto Hospitali ya Taifa Muhimbili Dkt. Victor Ngota alieleza kuwa upasuaji wa kuwatenganisha watoto unahitaji utaalamu wa hali ya juu hivyo ulihusisha jopo la wataalamu mbalimbali ikiwemo madaktari bingwa ikiwemo wa upasuaji watoto, upasuaji rekebishi, wataalamu wa usingizi ,wataalamu wa lishe pamoja na wataalamu wa radiolojia.

“ Tuliwapokea watoto hawa tarehe 11 Machi 2023 hivyo tulianza mchakato wa kuwahusisha wataalamu ambao wanahusika na huduma hizi, ilituchukua takribani muda wa miezi kumi kuangalia mwenendo wao wa afya kwa ujumla kabla ya kuwatenganisha ili kuweza kupata dira ya namna watakavyoishi mara baada ya kutenganishwa” amefafanua Dkt. Ngota.

Upasuaji huo umefanyika kwa muda wa takribani saa sita hadi kukamilika ambapo ni wa kwanza kufanywa na mdaktari wazawa hapa nchini na kuwa upasuaji wa nne kufanyika katika Hospitali ya Taifa Muhimbili.

# Wizara ya afya yapokea msaada wa trilioni 1.4 kutoka global fund



**Na. Cletus Sanga**
**Dodoma**

Serikali kupitia Wizara ya Afya imepokea msaada wa kiasi cha Tsh. Trilioni 1.4 kutoka Global FUND ili kutekeleza afua mbalimbali za UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria nchini kote kwa malengo endelevu ya Milenia ambayo yanakusudiwa kufikiwa ifika mwaka 2030.

Upokeaji wa msaada huo umefanyika chini ya Waziri wa Fedha Mhe. Mwigulu Nchemba na Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu kwa pamoja wameshuhudia utiji saini wa makabidhiano ya msaada huo baina ya Global Fund na Serikali ya Tanzania.

"Msaada huu wa fedha unalenga kutekeleza afua mbalimbali za UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria nchini kote lengo likiwa ni kutekeleza malengo endelevu ya Milenia ambayo yanakusudiwa kufikiwa ifika mwaka 2030". Alisema Waziri Ummy

Waziri Ummy aliwashukuru Global Fund kwa msaada huo mkubwa katika Sekta ya Afya na kwa kuridhia ombi la Sekta ya Afya kutumia frdha za msaada kutoka Global Fund kwa ajili ya kusomesha na kuwaajili wataalam wa Afya ngazi ya jamii (Community Health Workers) wapatao elfu Tano kwa kipindi cha miaka Mitatu ijayo ambapo wataalam hawa watasaidia kuleta mabadiliko ya utoaji wa huduma za Afya nchini.

Kwa upande wake Mkuu wa Global Fund katika sehemu ya High Impact Africa 2 Bw. Linden Morrison ameipongeza Tanzania kwa kushika nafasi ya Nne Kati ya nchi zinazopokea fedha hizo kutoka Global Fund.

"Lakini pia naipongeza Tanzania kwa kuendelea kutumia vizuri fedha hizo za msaada kutoka GLOBAL FUND ambapo Tanzania imefikia asilimia 92 ya utumiaji wa fedha hizo na hali hii inapelekea kuzifikia afua nyingi katika maeneo ya Kifua Kikuu, UKIMWI nà Malaria". Amesema Bw. Morrison.



## ASANTE KWA FOLLOWERS

# 500,000

**KATIKA UKURASA WA INSTAGRAM WA @WIZARA_AFYATZ**

**Tuendelee kukua pamoja Taifa lenye Afya Njema**
**#Tunaboresha Afya #MtuniAfya #AfyaniMtaji**




**Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**WIZARA YA AFYA, TANZANIA, TOLEO LA MWEZI JANUARI, 2024**